TANGAZO LA SERIKALI NA. 338 la tarehe 5/5/2023

SHERIA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA YA 272)

_____

AMRI

_____

(Imetoleewa chini ya kifungu cha 29(d))

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA ARUSHA (ARUSHA WSSA) YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mamlaka ya Maji safi na Usafi wa Mazingira Arusha (Arusha WSSA) ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2023.

Marekebisho ya bei

2. Bei za maji safi na usafi wa mazingira za Arusha WSSA zinarekebishwa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitakuwa na masharti yafuatayo:

(a) mnamo au kabla ya tarehe 30 Juni 2023 Arusha WSSA itawasilisha EWURA mpango wake wa biashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(b) mnamo au kabla ya tarehe 30 Juni 2023 Arusha WSSA itawasilisha EWURA mkataba wa huduma kwa mteja uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na viwango vya huduma vilivyooneshwa kwenye Mpango wa Biashara.

(c) mnamo au kabla ya tarehe 30 Juni 2023 Arusha WSSA itawasilisha ushahidi kwa EWURA kuwa imewajulisha wateja wake na kutoa elimu ya kutosha kwa wadau wake kama vile wateja, viongozi wa serikali, viongozi wa vyama vya siasa, wawakilishi wa taasisi za dini kuhusu mabadiliko ya bei za

huduma;

(d) Arusha WSSA itatekeleza matakwa ya tozo ya udhibiti kwa kuwasilisha tozo zilizokusanywa kwa wakati;

(e) Arusha WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(f) Arusha WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu;

(g) Arusha WSSA, kila mwaka na kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya Bei; na

(h) Arusha WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Arusha WSSA ikilinganishwa na mamlaka nyingine za maji safi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake.

Kufutwa kwa Amri T.S. Na. 799 la 2018

4. Amri ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (Arusha WSSA) ya Bei za Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2018 inafutwa.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa	
		2022/23 na 2023/24	2024/25
Majumbani			
0 to 5	1,330	1,840	1,850
>5 <15	1,550		
>15	1,810		
Wastani wa bei ya Majumbani	1,528		
Taasisi	1,510	1,820	1,830
Biashara	1,930	2,300	2,340
Viwanda	2,560	3,080	3,100
Viwanda vya vinywaji	15,300		
Wastani wa bei ya Viwanda	4,104		
Magati	1,000	1,000	1,000
Wastani wa bei	1,759	2,122	2,126

Bei za Majitaka za Sasa na Zilizoidhinishwa (Shilingi kwa Mita ya Ujazo wa Majisafi)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa	
		2022/23 na 2023/24	2024/25
Majumbani	375	490	500
Taasisi	510	765	780

Tangazo la Serikali Na. 338 (Linaendelea)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa	
		2022/23 na 2023/24	2024/25
Biashara	750	860	860
Viwanda	870	1,070	1,070

Bei za Maunganisho Mapya za Sasa na Zilizoidhinishwa (Shilingi kwa Maunganisho Mapya)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa	
		2022/23 na 2023/24	2024/25
Majumbani	15,000	15,000	15,000
Taasisi	19,000	19,000	19,000
Biashara	20,000	20,000	20,000
Viwanda	26,000	26,000	26,000

Bei za Boza za Sasa na Zilizoidhinishwa (Shilingi kwa Maunganisho Mapya)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa	
		2022/23 na 2023/24	2024/25
		TZS/Tripu	
Arusha City & Ngaramtoni			
Ujazo wa Maji ($10M^3$)	112,360	112,360	112,360
Ujazo wa Maji ($5M^3$)	89,900	89,900	89,900
Longido Town			
Ujazo wa Maji ($10M^3$)		112,360	112,360
Ujazo wa Maji ($5M^3$)		89,900	89,900
Usa River Town			
Ujazo wa Maji ($10M^3$)		112,360	112,360
Ujazo wa Maji ($5M^3$)		89,900	89,900
Monduli Town			
Ujazo wa Maji ($10M^3$)		112,360	112,360
Ujazo wa Maji ($5M^3$)		89,900	89,900

Bei za Kuondoa Majitaka za Sasa na Zilizoidhinishwa (Shilingi kwa kila tripu)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa	
		2022/23 na 2023/24	2024/25
Arusha City & Ngaramtoni			
Ujazo wa Gari ($10M^3$)	89,900	89,900	89,900
Ujazo wa Gari ($5M^3$)	73,000	73,000	73,000
Longido Town			
Ujazo wa Gari ($10M^3$)		89,900	89,900
Ujazo wa Gari ($5M^3$)		73,000	73,000
Usa River Town			
Ujazo wa Gari ($10M^3$)		89,900	89,900
Ujazo wa Gari ($5M^3$)		73,000	73,000
Monduli Town			
Ujazo wa Gari ($10M^3$)		89,900	89,900
Ujazo wa Gari ($5M^3$)		73,000	73,000

Bei za Sasa na Zilizoidhinishwa (Shilingi kwa kila tripu) za Kutupa Majitaka katika Mabwawa Maalumu ya Kutibu majitaka

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa	
		2022/23 na 2023/24	2024/25
Bei (TZS)	9,186	9,186	9,186

Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Maunganisho Mapya ya Maji (Shilingi kwa Maunganisho)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa	
		2022/23 na 2023/24	2024/25
Maunganisho Mapya ya Majitaka	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho	26,000	26,000
Maunganisho Mapya ya Majitaka	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho	26,000	26,000

JEDWALI LA PILI

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(e))

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA (KIASI SHILINGI MILIONI)

Na.	Maelezo ya Miladi itakayofanyika	2022/23	2023/24	2024/25
1	Ujenzi wa vyanzo viwili vya maji maeneo ya Benett na Lengine Juu-Monduli katika Mlima Longido ifikapo Juni 2023	107	-	-
2	Kukarabati vyanzo vya maji (chanzo cha Lolomsikio kilichopo Monduli (2024/25), Ngaresero (2023/24), Nurangima-Usa River (2024/25), Kiranyi (2022/23), Saiteru (2024/25), Sekei -Ngaramtoni (2023/24), na visima vya Ngaramtoni (2022/23) vinavyohudumia Monduli) ifikapo Juni 2025	121	121	121
3	Kukarabati matenki ya maji (Tenki la Hospitali la ukubwa wa mita za ujazo 90m lililopo Mlima Meru (2022/23), DikDik2-100m^3 (2023/24), Magadirisho-90m^3 (2024/25), engikareti 45m^3 (2023/24) na ujenzi wa uzio kwa matenki mawili (45m^3,50m^3) yaliyopo Longido Mlimani (2023/24-2024/25)) ifikapo Juni 2025	15	15	9
4	Ujenzi wa uzio (katika chanzo cha maji cha Kiranyi (2023/2024), ujenzi wa uzio katika chanzo cha maji cha Sekei (2022/2023), Ngaramton, ujenzi wa uzio katika tenki la Engikareti lenye mita za ujazo 45 (2022/2023), ujenzi wa uzio Mto Simba (2923/2024) na ujenzi wa uzio kwenye tenki la Mlima Longido (2023/24)) ifikapo Juni 2025	10	25	-
5	Kuamisha mabomba ya maji yaliopita katika makazi (inchi 3 kwa 1.7km kutoka katika chanzo cha maji cha Kiranyi (2023/24) na inchi 8 mabomba ya UPvC kwa 700m eneo la Longido (2022/23) ifikapo mwezi Juni 2023	41	120	-
6	Kufunga dira kubwa 33 kwenye vyanzo vyote vya maji na matanki ya kuhifadhia maji (dira 5 maeneo ya arusha (2024/25)), dira 3 maeneo ya Usa River (2022/23), dira 15 maeneo ya Ngaramtoni (2023/24-5& 2024/25 na dira 10 eneo la Monduli ifikapo Juni 2025	10	10	10
7	Kujenga matenki mapya 5 kwenye vituo vya kusukuma maji na vituo vya kusukuma mjai katika maeneo ya Kmandolu, Kiranyi, Kijenge, Moivo na Sanawari ifikapo Juni 2025	-	-	1,152
8	Kufanya utafiti wa ujenzi wa bwawa maeneo ya Weruweru ifikapo Juni 2025	-	-	1,000
9	Kubadilisha pampu 5 za kutibia maji kila mwaka, tatu (3) maeneo ya Oligilai, mbili (2) maeneo ya Sekei na bomba kumi (10) za kutibia maji katika	27	27	27

Tangazo la Serikali Na. 338 (Linaendelea)

Na.	Maelezo ya Miladi itakayofanyika	2022/23	2023/24	2024/25
	maeneo ya Midawe, Moshono, Loruvani, Ngarendolu, Kilimani, Tembo club, Burka na kwenye maeneo ya Olosiva ifikapo Juni 2025			
10	Kuendesha zoezi la usafishaji wa visima, kamera na kubadilisha pampu 10 maeneo ya Oltulelei, Iikiurei, Loruvani No 4, Old Sanawari, Kiranyi 1, Kata ya Loruvan, Sombetini, LongIdo, Ngusero na visima vya Misouri ifikapo Juni 2025	117	117	117
11	Ujenzi wa miundombinu ya maji 10.69km ya bomba kuu (3.5km kutoka chanzo cha Kolomonike mpaka kwenye tenki la Mashariki Mlimani - Monduli, kilomita 3.5 kutoka Kolomonike2 mpaka tanki la Lengine juu na kilomita 2.5 kutoka chanzo cha Olarash mpaka tanki la kijiji cha Olarash. Kilomita 1.054 kutoka Ngaresero mpaka tanki la Dikdik, mita 136 kutoka Nurangina mpaka tanki jipya la USA-River) ifikapo Juni 2025	-	37	75
12	Ujenzi wa miundombinu ya maji kilomita 453.829 kwa ukubwa wa inchi moja na nusu hadi 6 (kilomita 200 maeneo ya Arusha, kilomita 30.561 maeneo ya Ngaramtoni, kilomita 73.268 maeneo ya Usa-River, kilomita 55 maeneo ya Longido, kilomita 95 maeneo ya Monduli) (wastani wa kilomita 90.7658 kwa kila mwaka) ifikapo Juni 2025	1,652	665	614
13	Ujenzi wa bomba kubwa la maji lenye urefu wa kilomita 30 kutoka kwenye tenki la Ngorubob mpaka Monduli ifikapo Juni 2024	-	478	-
14	Kujenga matanki ya maji na miundombinu ya kutibia maji. Matenki matatu maeneo ya Monduli, ujenzi wa tenki la maji lenye ujazo wa mita 500 maeneo ya mashariki mlimani, ujenzi wa tenki lenye ujazo wa mita 500 Mlimani magharibi na ujenzi wa tenki la maji lenye ujazo mita 300 eneo la Lengine juu. Ujenzi wa tank la maji lenye ujazo wa mita 1000 na 500 maeneo ya Nurangima 1000 na Sekei ifikapo Juni 2025	-	795	-
15	Kuunganisha wateja wapya 41,978 (wateja 13,933 kwa kila mwaka) ifikapo Juni 2025	1,539	1,539	1,539
16	Kufanya uchunguzi na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa mtandao wa majitaka katika eneo la Kisongo ifikapo Juni 2025	-	-	103
17	Ununuzi wa ardhi kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji taka katika maeneo ya Monduli, Longido na Usa-River (ekari moja kwa kila eneo) ifikapo Juni 2025	-	-	900
18	Kufanya uchunguzi na usanifu kwa ajili ya ujenzi wa mtandao wa maji taka katika maeneo ya Monduli, Longido na Usa-River ifikapo mwezi wa sita 2025	-	-	158

Tangazo la Serikali Na. 338 (Linaendelea)

Na.	Maelezo ya Miladi itakayofanyika	2022/23	2023/24	2024/25
19	Kujenga mtandao mpya wa maji taka wenye urefu wa kilomita 30 (10km kwa kila mwaka) ifikapo Juni 2025	1,023	1,023	1,023
20	Ukarabati mfumo wa maji taka wenye urefu wa kilomita 100 (ukubwa wa inchi 8 na 6 maeneo ya Unga Ltd, Daraja II na Mjini kati) kila mwaka	46	46	46
21	Kufanya utafiti wa majaribio juu ya mfumo wa kielotroniki kwenye miundombinu ya maji taka ifikapo Juni 2023	15	-	-
22	Kufunga mfumo wa kidigitali wa kuongoza magri ya kubebea maji (boza) ifikapo Juni 2024	-	4	-
23	Kujenga chemba 17 za valvu na kubalisha chemba 12 kila mwaka	10	11	11
24	Kubadilisha mita 60,000 za wateja.	1,100	2,750	2,750
25	Kukarabati mabomba ya maji yaliyochakaa yenye urefu wa kilomita 160 katika maeneo ya Ngarenaro, Sakina, Engutoto, Daraja II, Lemara, Engosharaton, Sinoni, Unga Ltd, Osunyai na Sombetini.	605	1,816	2,421
26	Kuondoa mtando wa mabomba yaliyoingiliana yenye urefu wa kilomita 30 katika maeneo ya Ungalimited, Olmatejoo, Uswahilini, Baraa na Moshono kila mwaka.	-	516	258
27	Kubadilisha mabomba ya kuwaunganisha wateja yenye kipenyo cha inchi 3/4 hadi 1 zenye urefu wa kilomita 70.14 kila mwaka (Arusha 54km, 6km Ngaramtoni, 2.14 Longido, 6km Monduli, 2km Usa-River) ifikapo Juni , 2025	204	204	204
28	Kuanzisha na kusimamia uendeshaji wa kanda za mfumo wa maji (DMAs) katika jiji la Arusha kwa kufunga mita kubwa 5 kila mwaka	-	10	6
29	Kuanzisha mifumo ya kikanda ya maji (DMAs) kwenye kanda (8 maeneo ya Monduli, 4 maeneo ya Longido, 13 Maeneo ya Ngaramton na 4 maeneo ya Usa River) ifikapo Juni 2023	9	-	-
30	Kuanzisha mfumo wa usimamizi uhusiano wa wateja ifikapo Juni 2023	12	7	7
31	Kufanya utafiti wa majaribio (utoaji wa ankara wa papo kwa hapo) kwenye ofisi mbili za kanda ifikapo Juni 2024	-	4	-
32	Kufanya utafiti wa majaribio ya usomaji wa dira za kidigitali kwenye ofisi mbili za kanda ifikapo Juni 2024	13	5	5
33	Kufanya utafit wa majaribio juu ya mfumo wa usimamizi wa usomaji wa dira za maji kidigitali katika ofisi mbili za kanda ifikapo Juni 2025	-	7	-
34	Kufunga mita 200 za malipo kabla ya kupata huduma ya maji kila mwaka	55	55	55
35	Ununuzi wa komputa 36 and vifaa vyake (komputa 12 kila mwaka) kwenye ofisi za kanda ifikapo Juni	23	23	23

Tangazo la Serikali Na. 338 (Linaendelea)

Na.	Maelezo ya Miladi itakayofanyika	2022/23	2023/24	2024/25
	2025			
36	Ununuzi wa vichapishaji 9 na vifaa (vichapishaji 3 kwa kila mwaka) kwenye ofisi za kanda ifikapo Juni 2025	8	8	8
37	Ununuzi wa samani za ofisi kwenye ofisi za kanda ifikapo Juni 2024	132	132	132
38	Kununua ardhi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za kanda maeneo ya Monduli na Usa-River(eka moja kwa kila eneo) ifikapo Julai 2023	298	-	-
39	Kujenga nyumba za makazi ya ndaji na ofisi za kanda maeneo ya Ngaramtoni, Longido, Monduli na Usa-River ifikapo Juni 2025	229	1,409	1,409
40	Ununuzi wa pikipiki 15 na bajaji 15 kwa ajili ya ofisi za kanda (10 kwa mwaka wa kwanza na 20 kwa mwaka unaofuata) ifikapo Juni 2024	64	150	-
41	Kuwezesha ununuzi wa zana za kiufundi za kufanyia kazi (HDPE fusion machine 5, pampu za maji zinazobebeka 5 na kompresa zinazobebeka 5) ifikapo Juni 2024	72	48	-
42	Kuwezesha ujenzi wa uwanja wa michezo na sehemu ya mazoezi (GYM) ifikapo Juni 2025	-	250	-
43	Kuanzisha mfumo wa usimamizi wa fedha wa serikali na uhasibu ifikapo Juni 2023	13	5	5
44	Kufunga mfumo wa serikali wa ofisi wa kietroniki (mtandao-serikali, ofisi ya kielotroniki, vifaa vya kimtandao kama WAN Router, IPBX, IP Phones) ifikapo Juni 2023	76	5	5
45	Kufunga mfumo wa ukaguzi wa taarifa ifikapo Juni 2023	38	5	5
46	Kufunga mtandao wa komputa na kuunganisha mtandao katika ofisi za kanda ifikapo Juni 2023	38	-	-
47	Kuanzisha kituo cha taarifa cha AUWSA ifikapo Juni 2023	-	12	-
48	Kushirikiana na VITENS na washirika wengine ili kuboresha uendeshaji na ukuzaji uwezo wa AUWSA (kuboresha mfumbo CIS na kuendeleza mfumo wa mgandamizo wa maji wa mtandao wa AUWSA, ubora wa maji, upotevu wa maji na uunganishaji wa maji kwa kaya masikini) ifikapo Juni 2025	-	320	306
49	Kununua genereta mbili kwa ajili ya uendeshaji kwenye vituo cha kusukuma maji ifikapo Juni 2023	-	15	-
50	Kufunga na kusimamia mfumo wa usimamizi wa taarifa za rasilimali watu ifikapo Juni 2025	18	2	2
51	Ununuzi wa magari matatu (aina ya Station wigon) na basi moja la wafanyakazi ifikapo Juni 2025.	410	180	180
52	Ujenzi wa Mradi mpya wenye umbali wa 17.3 Km kutoka kisima cha Sinya mpaka Namanga	-	-	8,192
53	Ujenzi wa miundombinu ya maji umbali wa kilomita 49 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya	-	1,600	-

Tangazo la Serikali Na. 338 (Linaendelea)

Na.	Maelezo ya Miladi itakayofanyika	2022/23	2023/24	2024/25
	Mererani			
54	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 29.20 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Mateves	-	1,350	-
55	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 54 ili kusogeza huduma ya maji mji wa Bondeni.	-	2,509	-
56	Ujenzi wa miundombinu ya maji umbali wa kilomita 110 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Muriet.	-	5,100	-
57	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 40.21 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Kiranyi	1,859	-	-
58	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 115 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Ngaramtoni juu	-	5,300	-
59	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 31.58 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Olmoti	-	1,460	-
60	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 32.44 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Olasiti	-	1,502	-
61	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 113.97 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Moshono	-	5,270	-
62	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 20.66 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Sanawari	-	955	-
63	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 31. 37 ili kusogeza huduma ya maji mji wa Bondeni.	-	-	1,450
64	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 45.21 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Muriet	-	-	2,091
65	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 38.93 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Kiranyi	-	-	1,800
66	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 28. 33 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Ngaramtoni juu	-	-	1,310
67	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 22.75 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Olmoti	-	-	1,052
68	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 24.61 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Olasiti	-	-	1,138
69	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 37.85 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Moshono	-	-	1,750
70	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa	-	-	799

Tangazo la Serikali Na. 338 (Linaendelea)

Na.	Maelezo ya Miladi itakayofanyika	2022/23	2023/24	2024/25
	kilomita 17.29 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Sanawari			
71	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 20.07 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Mateves	-	-	928
72	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 11.68 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Monduli	-	-	540
73	Ujenzi wa miundo mbinu ya maji umbali wa kilomita 10. 60 ili kusogeza huduma ya maji maeneo ya Usa-River	-	-	490
74	ujenzi wa miundombinu ya maji umbali wa kilomita 22.04 kutoka Shangarai mpaka Moshono na tanki moja la maji	-	-	4,930
	Jumla	10,008	39,420	41,154

JEDWALI LA TATU

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(f))

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

Maelezo	Kizio	Lengo la Utendaji		
		2022/23	2023/24	2024/25
Maunganisho Mapya ya Majisafi	No.	13,993	13,993	13,993
Maunganisho Mapya ya Majitaka	**%**	3,200	3,200	3,200
Kiwango cha Upotevu wa Maji	**%**	34	28	25
Kiwango cha Kufunga Dira za Maji kwa Wateja	%	100	100	100
Ufanisi katika Ukusanyaji wa Mapato	%	94	96	98

Dodoma,
25 Aprili, 2023

JAMES A. MWAINYEKULE
Mkurugenzi Mkuu